**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**


***Unapojibu:***
***Mkuu wa shule***
***Mobile 0717053340***
***Email : Magambasec2007@gmail. Com.***

***SHULE YA SEKONDARI MAGAMBA,***
***S.L.B 99,***
***LUSHOTO.***


***KUMB. Na MGSS/JI/Fv/2024/24.***


**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0717 053 340**

**Makamu Mkuu wa Shule 0764 491 806 / 0716 463 104**

**Patron 0620 428 595**

**Shule ya Sekondari MAGAMBA**

**S.L.P 99- LUSHOTO**


**Tarehe 26/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**S.L.P ……………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAGAMBA HALMASHAURI YA LUSHOTO MKOA WA TANGA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya PCB / PCM

Shule ya Sekondari MAGAMBA ipo umbali wa Kilometa 13 Kaskazini mwa Mji wa LUSHOTO Usafiri wa basi kutoka mjini LUSHOTO unapatikana katika kituo cha magamba kilichopo karibu na benki ya NMB tawi la

LUSHOTO Nauli ni Shilingi elfu moja na mia tano(1500/=) kwa pikipiki ni Shilingi elfu tano (5000/=).

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/ 2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/07/2024

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

| Na. | SARE/MAHITAJI | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1 | Suruali mbili (2) rangi ya light blue za darasani zisizobana,zisizo na marinda na zenye mfuko mmoja wa nyuma na isiwe modo, iweze kuvuka goti bila kubana ikipandishwa juu. |  Ashoneshe popote |
| 2 | Mashati mawili (2) ya tetron special rangi nyeupe mikono mirefu | Anunue popote |
| 3 | Tai rangi ya light blue kwa ajili ya kuvaa darasani (rangi ni hiyo hapo juu ya suruali) | Ashoneshe popote |
| 4 | Tracksuit rangi ya dark blue | Anunue popote |
| 5 | Boshori la kuvaa kichwani wakati wa usiku kipindi cha baridi rangi ya bendera ya taifa | Anunue popote |
| 6 | Mkanda wa suruali wa kawaida rangi nyeusi | Anunue popote |
| 7 | Socks rangi nyeusi jozi mbili (2) au zaidi | Anunue popote |
| 8 | Masweta mawili (2) rangi ya kijivu kilichokolea | Anunue popote  |
| 9 | T- shirt moja | Inapatikana shuleni kwa bei ya shilingi15,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 10 | Nguo ya kushindia (shamba dress) ni Kaunda suti jozi mbili, iwe suruali na shati lenye kola, mikono mirefu rangi ni kijivu iliyokolea (aje akiwa amevaa jozi moja) |  Ashoneshe popote Lenye rangi ya kijivu iliyokolea inayoonekana kwenye picha |
| 11 | Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kufunga na kamba (visiwe buti au vyenye visigino virefu) | Anunue popote |
| 12 | Vifaa vya chakula ikiwa ni pamoja na sahani, kikombe na bakuli za aluminiamu na kijiko | Anunue popote |
| 13 | Picha nne (4) za Pasport size | Apige popote |
| 14 | Shuka mbili rangi ya blue, Godoro, blanketi moja kwa ajili ya baridi, foronya moja na chandarua moja | Anunue popote |
| 15 | Sanduku imara la bati (tranka) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyako liwe na kufuli | Anunue popote |
| 16 | Vifaa vya usafi ikiwa ni pamoja na ufagio wa nje wa kusimama, brashi ngumu ya kusugulia sakafu ya kusimama na brashi ngumu ndogo ya kusugulia sinki la choo, mopa ya kukaushia sakafu, ndoo mbili ndogo kwa ajili ya maji ya kunywa na usafi wako na jembe . | Anunue popote |
| 17 | Pullneck mbili rangi nyeusi (kuna baridi) | Anunue popote |
| 18 | Copy ya cheti cha kuzaliwa na results slips | Aje nazo |
| 19 | Bima ya afya na kama hana apatiwe kiasi cha fedha ya dharura kwa ajili ya matibabu akiwa shuleni | Aje nayo |

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

### (a) VIFAA VYA DARASANI

1. Ufike na daftari za kutosha (kuanzia Counter book 12, Quire 3 au 4) kwa ajili ya masomo yako, kalamu, penseli na mkebe (Mathematical Set)
2. Kikokotoo cha sayansi na Hisabati (Scientific Calculator) na calculator

hiyo iwe “non- programmable calculator”

3. Spring file mbili (2) za plastic
4. Koti la jeupe la mikono mirefu la maabara **(laboratory coat)**
5. Kwa wanafunzi wa PCB waje na **Dissecting kit moja (1)**
6. Kila mwanafunzi aje na rimu moja aina **ya Mondi No 1 Size A4** kwa **kila muhula wa masomo**

**(b) VITABU MUHIMU**

Ndugu mzazi/mlezi ili kuimarisha ufaulu bora kwa mwanao, unatakiwa umnunulie mwanao vitabu vifuatavyo muhimu vya rejea ( Waweza nunua kimoja au zaidi kwa kila somo kulingana na uwezo wako kifedha) kama vilivyoainishwa hapa chini

## PHYSICS

1. **S. CHAND’S, PRINCIPLE OF PHYSICS LASS XI (V.K MEHTA) (muhimu sana awe nacho)**
2. **S. CHAND’S, PRINCIPLE OF PHYSICS LASS XII (V.K MEHTA) (muhimu sana awe nacho)**
3. COMPREHENSIVE PHYSICS CLASS XI
4. COMPREHENSIVE PHYSICS CLASS XII
5. ROGER MUNCASTER
6. MODERN ABC

## CHEMISTRY

1. CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASS XI (DR S.K JAIN)
2. CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASS XII (DR S.K JAIN)
3. PHYSICAL CHEMISTRY, NGAIZA SERIES OF ADVANCED CHEMISTRY (NGAIZA LUSIMA)

## BIOLOGY

1. BIOLOGICAL SCIANCE, D.J TAYLOR (CAMBRIDGE UNIVERSITY PRESS)
2. UNDERSTANDING BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL, NELSON THORNES

## ADVANCED MATHEMATICS

1. ADVANCED LEVEL PURE MATHEMATICS,FOURTH EDITION (C.J TRANTER)
2. PURE MATHEMATICS I &2
3. UNDERSTANDING MATHEMATICS

## GENERAL STUDIES

4. TAFUTA KITABU CHA TIE KWENYE MTANDAO NA UPRINT KOPI YAKO
5. UNDERSTANDING GENERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL BY SOSPETER M. DEOGRATIUS

**(c) Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| Jumla | | 80,000/= |

Fedha zote ziwekwe kwenye akaunti namba
**41603100008, (MAGAMBA SECONDARY SCHOOL FUND ACCOUNT).**
Utapokelewa iwapo utakuwa umelipa michango hiyo na kukabidhi bank paying slip kwa Mhasibu wa shule.

**(d) Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**(e) Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

(f) Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**MUHIMU**

1. Mwanafunzi aje na risiti ya malipo ya benki (bank pay in slip –BPS)
2. Mwanafunzi atapokelewa tu iwapo amekamilisha kulipa michango na kukabidhi vifaa vyote vilivyoagizwa.
3. Mwanafunzi anashauriwa kuwa awe na fedha za mfukoni (pocket money)
4. Hakikisha unasoma kwa makini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Kama kuna sehemu hujaelewa uliza kwa walimu baada ya kuripoti.
5. Kuhusu vitabu vya kununua, mnunulie mwanafunzi angalau kitabu kimoja na kuendelea kwa kila somo

**HITIMISHO**

1. Kufeli au kutofanya mtihani kwa mwanafunzi bila taarifa maalum ni kosa kubwa sana lisilo la kuvumilika.
2. Tukumbuke kuwa serikali yetu imefuta ada ila majukumu mengine yanayomuhusu mzazi yanabaki kwa mzazi

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAGAMBA**



**PETER M NYELLO**
**MKUU WA SHULE**




**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0717 053 340**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0764 491 806 / 0716 463 104**
- **Mwandamizi Taaluma 0716 114 386**
- Mwandamizi Malezi 0620 428 595

**KIAMBATISHO A**

# ***HISTORIA FUPI YA MWANAFUNZI (PERSONAL PARTICULARS)***

***SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI***

| PICHA YA MWANAFUNZI |
|---|

1. Jina kamili la mwanafunzi ___________________________________________
   (a) Tarehe ya kuzaliwa ____________________________________________
   (b) Kijiji / mtaa alichozaliwa/Mji ________________wilaya ________________
   Dini /dhehebu__________________________________________________
   URAIA __________________________________________________________

2. (a) Shule ya sekondari uliyotoka _________________________________________
   Anuani ya shule ya sekondari uliyotoka _______________________________

| PICHA YA MZAZI/MLEZI |
|---|

3. (b) Jina kamili baba /Mlezi ……………………………UHUSIANO_______________
   (c) Hai/Amefariki ___________________________________________________
   (d) Anuani ya Mzazi/Mlezi _____________________________________________
   (e) Mahali anapoishi …………………………………mtaa wa__________________
   Kazi anayofanya _________________________________________________
   (f) Jina la atakayekulipia karo________________________________________
   Anuani yake_____________________________________________________
4. **AFYA**: (i) Taja magonjwa yote makubwa yaliyowahi kukushika (k.m kifafa, pumu, kifua kikuu ) ______________________________________________________
   (ii) Unaupungufu au matatizo yoyote ya viungo (mfano macho, kilema n.k.) _____
   ______________________________________________________________________

***SEHEMU YA PILI: UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI***

Ninathibitisha kwamba maelezo aliyoyatoa mwanafunzi katika karatasi yote ni sahihi.

***Jina la Mzazi/Mlezi*** ______________________________________________________

***NAMBA YA SIMU YA MKONONI***_______________________________________________

SAHIHI___________________________________TAREHE______________________________

***SEHEMU YA TATU: UTHIBITISHO WA AFISA MTENDAJI KATA***

**Ninathibitisha kuwa mwanafunzi mtajwa hapo juu ni raia wa Tanzania na anaishi ndani ya kata hii.**

Jina la Afisa Mtendaji_________________ KATA YA________________________________

SAHIHI______________________________TAREHE__________________________

Tarehe …………………………………

## KIAMBATANISHO B

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PO-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

## ***REQUEST OF MEDICAL EXAMINATION***

**MAGAMBA SEC. SCHOOL,**
**P.O.BOX 99,**
**LUSHOTO**

**TO MEDICAL OFFICER.**
**……………………………………**
**…………………………………….**
**……………………………………**

**REF: STUDENT MEDICAL EXAMINATION FORM**

**Please Examine student named ………………………………………………………………………………in respect of these areas and any other areas(S) deemed relevant in connection to whether the student has problems related to**

**(a) Sight Yes/No. If yes, state………………………………………………………………………………………….**

**…………………………………………………………………………………………………………………………**

**(b). Hearing Yes/No If yes, state…………………………………………………………………………………**

**…………………………………………………………………………………………………………………………**

**(c ). T.B. or any other chronic Diseases. Yes/No If yes, state……………………………………………….**

**……………………………………………………………………………………………………………………………**

**…………………………………………………………………………………………………………………………**

**(d) Blood pressure. Yes/No If yes, state………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………………………………………**

**(e) Any physical impairment(s). Yes/No If yes, state…………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………………………………………**

**Do you therefore recommend this pupil to pursuer studies at this school?.**

**…………………………………………………………………………………………………………………………………**
**…………………………………………………………………………………………………………………………………**
**…………………………………………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………………………………………….**

**Name……………………………………………………… signature…………………………………date………………**
**Official title…………………………………………………… Official stamp**

**KIAMBATISHO C**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAISI – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**
**SHULE YA SEKONDARI MAGAMBA, S.L.P 99, LUSHOTO**
**KUMB. Na MGSS/JI/Fv/2023/24**
**MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………………………. …………**

**<u>YAH: MAELEZO YA MKATABA WA KUKUBALI NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MAGAMBA MWAKA 2023/24</u>**

**Fuata panapohusika**

**<u>SEHEMU YA MZAZI/MLEZI</u>**

1. Mimi mzazi/mlezi wa……………………………………………….......................

   Nakubali/sikubali nafasi ya kujiunga na kidato cha Tano katika shule ya sekondari Magamba 2023/24 kwa sababu ………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………….
   ……………………………………………………………………………………………… Naahidi nitatimiza/sitatimiza mahitaji yote muhimu kwa ajili ya kummwezesha mwanangu kuendelea na masomo katika kipindi chote atakachokuwa hapo shuleni. Aidha naahidi kuwa nitamshauri vizuri mwanangu hasahasa wakati wa likizo kuhusu mwenendo bora wa kitabia ili afanikiwe katika masomo na hatimaye kuwa raia mwema na mwenye ushirikiano na uzalendo.

   Jina langu……………………………………..Saini …………………… Tarehe……..

2. Mimi (mwanafunzi)………………………………………………………… ambaye nimechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Magamba tahasusi ya …….. nakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Magamba. **Naahidi nitatimiza na kufuata kanuni, taratibu na sheria zote zilizowekwa na shule na serikali ili niweze kuendelea na masomo kwa amani pia sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;**

   Jina langu……………………………………..Saini …………………… Tarehe……..

3. Maelezo haya yamethibitishwa/ yatathibitishwa na



**PETER MICHAEL NYELLO**
**MKUU WA SHULE**

